



**VARBERGS
KOMMUN**

Myenyekiti wa Bodi ya Manispaa Ann-Charlotte Stenkil na Mkurungenzi wa Manispaa Carl Bartler wameandika barua hii kwa watu wore wenyekuhishi mu Manispaa ya Varberg. Barua hii imepatikana pia mu varberg.se na mafasi zingine 2020-03-26

Barua kwa watu wenyekuhishi mu manispaa ya Varberg

Pamoja tunaweza kupunguza maambukizo na kuongeza usalama

Dunia imebadirika. Madhara ya coronavirus zinafika na zinagusa ma inchi zote. Maambukizo yanafanyika mbiyo sana kwa sababu hakuna vaccin na hakuna mtu mwenye amekuwa na uwezo ya kujikinga na virus hiyo.

Tunajuwa kama wengi wenye wanaambukizwa wako na kikohozi na homa. Tunajuwa pia kama uzee na magonjwa fulani zinaweza leta matokeyo ya hatari zaidi. Saa yote tunapata habari za mpya kuhusu maambukizo na magonjwa, na tunahusiyana na wasiwasi yenye kuwa mu jamii yetu.

Kwa kuzuiya hiyo virus tunapashwa kukamata ma uamuzi kubwa ile tupate matokeo ya kabambi na ya muzuri. Ma concert na mikutano ya mchezo zinakatazwa. Ma kampuni zinapashwa kufwata hii sheria ya mpya. Usafiri na mikutaniko zinakatazwa pia. Mauendeshaji zinasimamishwa na inchi inafunga mipaka (frontières) yake. Mu manispaa ya Varberg tunasimamisha mikutano zote na tunakataza watu watembeleye waze wenye wako ku manyumba ya waze na ku hospitali.

Jukumu yako ni muhimu

Ya muhimu kwako mwenye unaishi mu manispaa ya Varberg ni kusaidiwa kupunguza maambukizo. Kwa hiyo inalomba uwe na mikono safi, uheshimiye sheria yenye inakataza kutembeleya waze na kubakiya kunyumba kwako kama unagonjwa. Kama watoto wako wanagongwa wanapashwa bakiya kunyumba.

Weye mwenye uko na afya ya muzuri unaweza pia kusaidiwa ili usalamaa uongezeke mu jamii yetu. Sisi wote tunakuwa na wasiwasi, lakini inawezekana unajuwa mtu mwenye iko na wasiwasi ya mingi zaidi? Unaweza kusaidiwa ule mtu.



**VARBERGS
KOMMUN**

- Kama unajuwa mze moja karibu yako mwenye hana habari kuhusu coronavirus, unaweza kamata muda kidogo ile umufasiliye na umuelezeye yenye ikonapitikana mu dunia na mu manispaa yetu. Unaweza mununuliya chakula kidogo wakati unaenda kuemeya.
- Kama unajuwa jirani mwenye haongeye kiswidi, unaweza musaidiya na kumutafsiria yenye serikali na manispaa wanasema.
- Ukiona habari ya bongo mu réseaux sociaux, oneshu ukweli na eleza ile ukweli kwa serikali.
- Hepuka kutembeleyana na kututanana na watu, tumiya simu wala namna ingine ya kuongeya na watu.
- Tunajuwa kama mipango kama hii tayari imechukuliwa mu manispaa yetu. Yenye tunapenda ni kuona hii mipango iendeleye na kutimilika kwa kuongeza usalama na kupunguza maambukizo.

Jukumu yetu iko wazi

Sisi waongozi ya manispaa ya Varberg tunawahaidi kwamba tutajikaza sana kushugulikia mambo hii. Watumishi ya masomo, hospitali na mafasi zingine wanatuunga mukono. Watumishi yetu wana zoezi ya kutumika na utulivu, haraka na usafi. Hivi sasa wanafanya hatua.

Tuna kazi ya kubwa mbele yetu. Ndiyo maana tunapashwa kuwa na mipango na zoezi ile tuweze kutumika pamoja na tuwe na uwezo ya kukamata uamzi kwa haraka. Tunajikaza pia tuwafikishe ma habari yenye kuwa ya ukweli mbele ya wakati.

Kushugulikiana ni ya muhimu sana. Kama tunasaidiyana, tutaweza pamoja kuhepuka hatari hii katika siku zijazo.

Ann-Charlotte Stenkil

Mwenyekiti ya Bodi ya Manispaa ya Varberg

Carl Bartler

Mkurugenzi wa Manispaa ya Varberg